

Jilinde. Linda jamii yako. **Pata kuchanjwa.**



CHANJO ZA COVID-19: PATA KUJUA UKWELI

Chanjo inatolewa BILA MALIPO kwa watu wote.

Chanjo ni za bila malipo kwa kila mtu, bila kujali hali yako ya uhamiaji au kama una kitambulisho au bima ya matibabu.

Chanjo ni salama na yenye ufanisi. Chanjo HAIWEZI kukuambukiza COVID-19.

Katika historia ya Marekani, hakuna chanjo nyingine ambayo usalama wake umechunguzwa hivi.

Athari ni za kawaida.

Athari humaanisha kuwa chanjo inafunza mwili wako jinsi ya kupigana na COVID-19.

Hata ikiwa ulikuwa na COVID-19, bado unapaswa kupewa chanjo.

Kaa salama baada ya kuchanjwa na uendelee:

- Kuvala maski.
- Kuhakikisha hukaribiani na watu.
- Kunawa mikono yako mara kwa mara.
- Kusafisha sehemu zinazoguswa mara kwa mara.
- Pata chanjo kamili ya COVID-19, ikiwa ni pamoja na kupata dozi za kuimarisha kinga ya mwili unapostahiki.